PANDA MITI KIBIASHARA

PARTICIPATORY PLANTATION FORESTRY PROGRAMME

# PARTICIPATORY PLANTATION FORESTRY PROGRAMME

SHERIA NDOGO ZA KUZUIA NA KUSIMAMIA MOTO WA MSITUNI ZA HALMASHAURI YA KIJIJI/ MTAA CHA/WA................................................................................................ YA 2022

United Republic of Tanzania
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
Forestry and Beekeeping Division

Embassy of Finland
Dar es Salaam

**Dibaji**
Waraka huu ambao umeandaliwa kwa mashauriano kati ya serikali za mkoa wa Iringa, Njombe, Ruvuma, na wilaya ya Mufindi, unatoa kielelezo cha sheria ndogo kinachowezwa kuboreshwa kuendana na matakwa ya usimamizi na uzuiaji wa moto wa misituni.  Unakusudiwa kutoa mfumo wa kisheria wa usimamizi wa hatari za moto katika vijiji vyenye uwekezaji mkubwa wa mashamba ya misitu ya kupandwa.

Imekusudiwa kuwa mabaraza ya vijiji na mikutano mikuu ya kijiji yapitie kwa kina waraka huu na kuuboresha ili kukidhi mahitaji yao mahususi kabla ya kuupeleka kwa halmashauri zao za wilaya au miji ili kupitishwa.

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

SURA YA 287

HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA/WA**....................................................**

**SHERIA NDOGO**

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 168)

SHERIA NDOGO ZA KUZUIA NA KUSIMAMIA MOTO WA MSITUNI ZA HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA/WA.**.............................................** YA 2022

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jina na tarehe ya kuanza kutumika | 1. | | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Kuzuia na Kusimamia moto wa msituni za Kijiji/Mtaa **---------** za Mwaka 2022 na zitaanza kutumika baada ya kupitishwa na Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa ya **---------------------** |
| Eneo la kutumika | 2. | | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la kiutawala la Kijiji/ Mtaa cha/ wa**----------------------------------------------------** |
| Tafsiri | 3. | | Katika Sheria Ndogohizi, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo:-<br><br>**“Afisa Mwidhiniwa**” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>“**Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa**” maana yake ni mtu yeyote anayetekeleza majukumu ya Mtendaji wa Kijiji/Mtaa.<br><br>**“Mratibu wa Moto wa Msituni Wilaya/Mji/Manispaa”** ni Afisa wa ngazi ya juu anayeteuliwa na Mkurugenzi Wilaya/Mji/Manispaa kwa kushauriana na Mkuu wa Idara ya Maliasili, Utalii na Mazingira ili kusimamia masuala yote yahusuyo moto wa msituni na kuyatolea taarifa kwa Mkurugenzi Wilaya/Mji/Manispaa.<br><br>“**Ardhi ya Hatari”** ina maana ya ardhi ambayo kama isipotunzwa inaweza kuhatarisha maisha au kuharibu mali na mazingira.<br><br>**“Kelele”** ni uchafuzi wowote unaosababishwa na sauti ambayo ni chukizo kiasili na inaweza kusababisha athari hasi kwa afya ya binadamu na mazingira. |

“Halmashauri **ya Wilaya”** maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya **-----------------------------------------------------------------**

“**Halmashauri ya Kijiji/Mtaa”** maana yake ni Halmashauri ya KijijiMtaa cha/wa**----------------------------------------------------**-

**“Makazi”** inajumuisha nyumba, kiwanja na kila aina ya milki ikiwa ni pamoja na mashine, mitambo na vifaa vitumikavyo katika kazi zinazofanywa katika makazi hayo.

**“Mazingira”** neno mazingira linaweza kufafanuliwa kama jumla ya vitu vyote vilivyo hai na visivyo hai na athari zake chanya na hasi zinazoathiri maisha ya mwanadamu. Au neno mazingira ni hali ambayo mtu, mnyama au mmea huishi au kufanya kazi.

**Maeneo ya Hatari ya Moto "** ni maeneo ambayo ni rahisi kushika moto na yana wingi wa vitu viwakavyo.

**“Mifugo”** maana yake ni wanyama wa kufugwa wakiwemo ng’ombe, kondoo, mbuzi, nguruwe, kuku, farasi, punda na wanyama wengine wa kufugwa.

**“Misitu”** inajumuisha ardhi yote iliyofunikwa na uoto wenye miti mingi ya ukubwa tofauti ivunwayo na isiyovunwa. Pia inajumuisha miti ya asili na miti ya kigeni. Miti ya asili ina uwezo mkubwa wa kustahimili moto kulikoni miti ya kigeni.

“**Rasilimali za mazingira”** Rasilimali za mazingira” ni vitu vilivyo hai na visivyo hai vinavyojumuisha mazingira ya kibiofizikia ambayo yanaweza kutoa manufaa kwa binadamu. Zinajumuisha rasilimali za udongo (madini na nishati), rasilimali za kibayolojia, rasilimali za maji, rasilimali za hewa na rasilimali za ardhi.

**“Taka hatarishi”** maana yake ni taka ngumu, vimiminika au hewa ambayo ina kiasi kikubwa cha kemikali zinazoweza kusababisha sumu ambayo inaweza kuathiri maisha ya binadamu pamoja na mazingira kwa ujumla.

**“Uharibifu”** maana yake ni mabadiliko hasi aidha kwa uhai wa binadamu, mazingira au mali. Inaamanisha mabadiliko ya moja kwa moja kwa hali ya kimwili, joto, kemikali na kibayolojia ya rasilimali ambazo ni sehemu ya mazingira na hivyo inaweza kusababisha madhara kwa matumizi ya

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | manufaa ya rasilimali hizi, au kusababisha hali ambayo ni hatari kwa jamii, afya yake, usalama, ustawi wa binadamu au mazingira.<br><br>"**Udhibiti wa moto"** Maana yake ni kuweka moto chini ya udhibiti ili usiwezi kuenea tena. Haimaanishi kuwa moto utakuwa umekufa kabisa hapana, kwani bado utakuwa na uwezo na kufufuka tena na kuleta madhara hapo baadaye.<br><br>**"Kuzima moto" maana** yake ni mbinu zitumikazo katika kuzima moto ikiwa ni pamoja na kufanya shambulio la moja kwa moja katika kuzima moto au njia ya kutumia moto mdogo ili kuzima moto mkubwa<br>.<br>"**Mashambulizi ya moto sambamba"** maana yake ni njia inayotumika kuzima moto ambapo barabara au ufito unaotenga eneo lenye moto na lisilo na moto hutengenezwa takribani sambamba na ukingo wa moto. Lengo ni kuruhusu moto kuwaka kwa usalama katika eneo ambalo liko ndani ya mstari wa moto.<br><br>**"Usimamizi wa Moto"** neno usimamizi wa moto linajumuisha:<br>**Ulinzi wa moto:** hatua zote zinazochukuliwa kulinda mali. Baadhi ya mkakati hiyo ya kulinda mali ni pamoja na kuweka barabara za kuzuia moto, kuwa na wafanyakazi wenye maarifa na ujuzi, kununua vifaa na zana za kuzimia moto, uwepo wa mfumo wa FDI pamoja na sehemu za kuangalia moto kwa mbal, increase resilliance of assets, n.k<br>**Kuzuia moto**: maana yake kutambua sababu zote za moto na kisha kutafuta mbinu za kuzuia shughuli hizo ili kuepuka kutokea kwa moto usiohitajika. Shughuli ambazo ni chanzo cha moto usiohitajika ni pamoja na: kuwinda, kukusanya asali, uchomaji wa mkaa, kutengeneza matofali, kuwasha/kupika katika makambi ya wapasuaji wa mbao. Kinga hufanywa kupitia mchakato wa elimu/uhamasishaji, utekelezaji wa sheria na juhudi za kihandisi kutenga shughuli hatari kama vile kutengeneza mkaa.<br><br>**Kuzima moto:** shughuli zote zinazochangia kuzima moto (kuwa na timu ambayo iko tayari kwa mapambano muda wote kwa kutumia njia sahihi, kugeuza vijiinga vya moto na kuvimwagia maji na kisha kufanya ufuatiliaji ili kuwa na uhakika iwapo moto wote umekufa kabisa}. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | "**Kielezo cha Hatari ya Moto (FDI)"** Ni kitabiri cha uwezekano wa moto kuwa wa hatari kulingana na hali ya hewa ya siku hiyo (joto, unyevu na kasi ya upepo). FDI pia hutumika kama kigezo cha kuamua kuidhinisha au kutoidhinisha maombi ya kibali cha moto.<br><br>“**Kielezo cha Hali ya Hewa ya Moto**" ni kitabiri mbadala cha uwezekano wa moto kuwa hatari na sawa na FDI.<br><br>**“Inayoweza kuwaka”** Kitu chochote kinachoweza kushika moto ikiwa ni pamoja na mimea.<br><br>**“Kamati ya Maliasili”** maana yake ni Kamati iliyoundwa na Halmashauri ya Kijiji/Mtaa na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa kwa madhumuni ya kuhifadhi/kusimamia maliasili.<br><br>**"Maeneo ya Usalama"** maana yake ni eneo ambalo kwa kawaida halina mimea inayoweza kuwaka ambapo watu, magari na vifaa vinaweza kuwekwa kwa usalama wakati wa tukio la moto endapo upepo utabadilika au tabia ya moto isiyotarajiwa.<br><br>**“Moto Usiodhibitiwa”** maana maana yake ni moto usiokuwa na uangalizi maalum ambao bado unaenea kwa kasi. Ni vigumu kuuweka chini ya udhibiti moto usiodhibitiwa kutokana na ukali wake.<br><br>“**Wadau”** maana yake ni wamiliki wa mashamba pamoja na taasisi mbalimbali zinazojishughulisha na usimamizi wa moto. Pia wamiliki wa mashamba pamoja na taasisi hizo ni miongoni mwa wanufaika na kazi zinazofanywa za kusimamia matumizi bora ya moto.<br><br>"**Moto wa mwituni"** maana yake ni moto usiodhibitiwa ambao unaweza kuanzishwa kwa makusudi au bila kukusudia au moto huo unaweza kusababishwa na nguvu za asili kama vile radi.<br><br>“**Jumuiya”** maana yake ni kundi lolote la watu wakiwemo watoto, vijana, watu wazima, wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara, wafugaji, wavuvi, viongozi wa dini n.k wanaoishi katika kijiji/Mtaa cha/wa**………………………… .**<br><br>**“Baraza la Usuluhishi wa Migogoro la Kata”** maana yake ni Baraza la utatuzi wa migogoro la Kata ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **…………………………………………** Imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Kata ya mwaka 1985.<br><br>**“Faini**” maana yake ni adhabu iliyotolewa kwa mtu yeyote ambaye amethibitishwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.<br><br>“**Familia”** maana yake ni baba, mama na watoto wakiwemo watoto wa kuasili na ndugu wa damu au ndugu wa karibu wakiwemo babu, nyanya, wajomba, shangazi, binamu, wapwa wanaoishi katika kaya hiyo.<br><br>“**Kibali”** maana yake ni kibali au ruhusa iliyotolewa kwa maandishi Watendaji wa Kijiji/Mtaa au mtu yeyote anayekaimu shughuli za Watendaji wa Kijiji/mtaa kuruhusu shughuli fulani kutekelezwa.<br><br>“**Kwa kukusudia”** maana yake ni kufanya kitendo kwa makusudi huku ukijua kuwa kufanya kitendo hicho ni kinyume cha sheria.<br><br>“**Mazao”** maana yake ni mazao kutoka mashambani, misituni na mitoni.<br><br>“**Mkazi”** maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika Kijiji /Mtaa cha/wa **……………………………………**<br><br>**“Mkurugenzi**” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa ya **---------------------**<br><br>**"Mtoto"** maana yake ni mtu yeyote chini ya miaka 18.<br><br>“**Barabara ya kuzuia Moto”** maana yake ni eneo linaweza kupunguza kasi ya moto. Linaweza kuwa ni eneo la asili kama vile mito, matindiga na misitu ya asili ambayo haishiki moto kwa urahisi. Pia linaweza kuwa ni eneo ambalo limetengenezwa na binadamu kama vile njia za waenda kwa miguu, barabara za ng’ombe, barabara za magari, eneo lililolimwa, uwanja wa michezo nk.<br><br>“**Njia ya kujiokolea”** maana yake ni njia iliyoandaliwa ambayo hutumika kujiokoa kutoka kwenye moto hatari<br><br>“**Kibali cha Usimamizi wa Moto katika shughuli zinazohusiana na ardhi**” ni waraka rasmi wa Kijiji/Mtaa ambao unaruhusu matumizi yaliyodhibitiwa ya moto katika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kusafisha mabaki ya kilimo, uboreshaji wa malisho na kusafisha mabaki ya miti baada ya kuvuna. Shughuli hizo zinatekelezwa kwa mujibu wa Mpangokazi wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji/Mtaa<br><br>**“Kibali cha Usimamizi wa Moto wa Sekta za biashara Vijijini”** maana yake ni Kibali kinachotoa udhibiti wa matumizi ya moto katika uchomaji wa mkaa, uchomaji wa wa matofali pamoja na usimamizi wa bidhaa na taka zinazozalishwa na mashine za mbao zinazohamishika na zisizohamishika.<br><br>**"Kamati ya Kijiji/Mtaa ya Usimamizi wa Moto”** maana yake ni Kamati iliyoidhinishwa na Mkutano wa Kijiji/Mtaa kuchukua jukumu la Usimamizi wa Moto wa Kijiji/Mtaa.<br><br>**“Kikosi cha Kuzima Moto cha Kijiji/Mtaa”** maana yake ni kikundi cha Wanakijiji/Mtaa walioidhinishwa na Serikali ya Kijiji/Mtaa ambacho hufanya kazi zake za kudhibiti moto kwa kusimamiwa na Kamati ya Kijiji/Mtaa ya usimamizi wa Moto. Kwa kawaida, Kikosi cha Kuzima Moto kina wajumbe 15.<br><br>**“Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa** maana yake ni mfuko wa moto ulio chini ya udhibiti wa Serikali ya Kijiji/Mtaa na Kamati ya Usimamizi wa Moto. Lengo la Mfuko huo ni kutumika katika kazi za usimamizi wa moto.<br><br>**Mpangokazi wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji/Mtaa**” maana yake ni mpangokazi ulioidhinishwa na Mkutano wa Kijiji/Mtaa unaoelezea shughuli za usimamizi wa moto ikiwa ni pamoja na kulinda, kuzuia na kuzima moto. Mpangokazi huo pamoja na bajeti hupitiwa upya kila baada ya mwaka mmoja ili iendane na mahitaji ya jamii husika. Uc<br><br>**“Uchomaji moto uliopangwa”** maana yake ni moto ambao unawekwa chini ya uangalizi maalum lengo likiwa ni kupunguza mzigo wa viwako msituni au kuboresha malisho ya wanyamapori na mifugo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kuwasha moto** | **4.** | (1) | Ni marufuku kwa mtu yeyote kuwasha moto katika eneo la wazi, msitu wa asili au shamba la miti midogo au mikubwa bila Kibali au kama FDI itakuwa zaidi ya 55 kwa siku hiyo. |
| | | (2) | Mtu yeyote ambaye atawasha moto bila kibali kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa au Afisa mwingine aliyeidhinishwa, au kama FDI itakuwa juu ya 55 au kama hatajaribu kuzuia moto huo usisambae, atakuwa anatenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi |
| | | (3) | Kibali cha kutumia moto kwa ajili ya utayarishaji wa mashamba na shughuli za uzalishaji mali Kijijini kama vile kuchomaji mkaa, kuchoma matofali na kuchoma mabaki ya viwanda vya upasuaji mbao au uchomaji mwingine kama huo kitatolewa na Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa au Afisa mwingine aliyeidhinishwa baada ya Kamati kujiridhisha kuwa mwombaji/waombaji wa kibali hicho amekidhi/wamekidhi vigezo muhimu kama vilivyoambatanishwa kwenye **Jedwali la Kwanza** la Sheria Ndogo hizi. |
| | | (4) | Iwapo mtu mwenye kibali cha kuchoma moto atashindwa kuchoma shamba lake katika siku iliyopangwa, atalazimika kuomba kibali kingine bila malipo yoyote kwa mujibu wa masharti yaliyomo kwenye Sheria Ndogo hizi |
| | | (5) | Bila ya kuathiri masharti yoyote katika Sheria Ndogo hizi, Kibali cha kutumia moto kama kitakavyokubaliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa hakitazidi malipo ya TZS 2,000. |
| | | (6) | Ili kuboresha rutuba, kudumisha unyevunyevu, na kudhibiti matukio ya moto holela, ruhusa ya kuwasha moto kuchoma takataka/nyasi/mashina/ mabaki yoyote wakati wa utayarishaji wa mashamba ya kilimo haitatolewa, hadi itakapothibitishwa na Kamati kuwa kuna haja ya kutumia moto ili kuondosha taka hizo shambani. |
| | | (7) | Kila mmiliki au Mtu aliyekodisha shamba kwa ajili ya kilimo cha mazao ya chakula, mazao ya biashara, ardhi ya malisho, miti ya biashara au miti ya asili atakuwa na wajibu wa kuweka barabara za kuzuia moto kuzunguka shamba/eneo lake kabla ya tarehe 30 Juni au tarehe nyingineyo itakayopitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Upana wa barabara za moto utakuwa ni mita 2.5 kwa kila upande na hivyo kufanya jumla ya Mita 5 kwa pande zote mbili kati ya shamba na shamba. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (8) | Mmiliki au Mtu aliyekodisha shamba atakayeshindwa kuweka barabara ya kuzuia moto kuzunguka shamba/eneo lake kwa muda uliotajwa hapo juu atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi. |
| | | (9) | Litakuwa jukumu la kila mzazi/mlezi kuhakikisha kwamba watoto wao hachezei moto au hawajihusishi na vitendo vya kuwasha moto. Wazazi/walezi watawajibika kwa uharibifu wowote utakaosababishwa na moto uliowashwa na watoto wao kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi.<br>Watu watakaosababisha moto kwa sababu ya uvutaji sigara watakuwa wametenda kosa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi. |
| | | (10) | Watu watakaosababisha moto kutokana na uvutaji sigara watakuwa wanatenda kosa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi |
| | | (11) | Watu watakaosababisha moto kutokana na shughuli za uwindaji watakuwa wanatenda kosa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi. |
| | | (12) | Watu watakaosababisha moto kutokana na shughuli za uvunaji na usindikaji wa asali watakuwa wanatenda kosa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi. |
| Ruhusa ya kutumia Moto katika matumizi ya usimamizi wa ardhi | 5 | (1) | Kibali cha kutumia moto kwa ajili ya matumizi ya usimamizi wa ardhi (kusafisha mashamba ya kilimo, kuboresha malisho ya mifugo na kuchoma taka za mabaki ya upasuaji wa mbao) kitatolewa iwapo tu masharti yafuatayo yatatimizwa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi.<br>1) Iwapo kielelezo cha FDI kitakuwa chini ya 55 kwa muda wa siku tatu mfululizo. FDI chini ya 55 inaonyesha kwamba ndani ya siku hizo kasi ya upepo, halijoto na kiasi cha unyevunyevu angani ni salama kwa kuwasha moto.<br>2) Mwombaji wa Kibali atatakiwa kuweka barabara za kuzuia moto zenye upana usiopungua Mita 5 kuzunguka shamba/eneo lake ili kuzuia uwezekano wa moto kutoroka. Ikumbukwe kwamba tarehe ya mwisho ya kuweka barabara za kuzuia moto ni tarehe 30 Juni au tarehe nyingineyo itakayopendekezwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | 3) Iwapo Mwombaji atatimiza masharti fungamano yafuatayo:<br>a) Angalau kuwa na wasaidizi sita wa kusaidia katika kudhibiti moto endapo utaonyesha dalili za kutoroka.<br>b) Kuwa na vifaa na zana za kuzuia au kudhibiti moto;<br>c) Uwepo wa vyanzo maalum na vya kutosha vya maji;<br>d) Kuwa tayari kukagua na kulinda eneo lililowashwa moto kwa muda wa siku saba (7) mfululizo iwapo kama taka zilizochomwa moto ni matawi ya miti iliyovunwa na masalia ya upasuaji mbao<br>e) Kuwa tayari kukagua na kulinda eneo lililowashwa moto kwa muda wa siku mbili (2) mfululizo iwapo kama taka zilizochomwa moto ni nyasi au taka za shamba lililovunwa mazao;<br>f) Kutoa taarifa kwa majirani juu ya kusudio la kuchoma moto angalau siku tatu (3) kabla ya uchomaji uliokusudiwa;<br>g) Moto utakaowashwa ni kwa mujibu wa Mpango kazi wa Usimamizi wa Matumizi Bora ya Moto;<br>h) Kulipa ada ya maombi ya kibali cha kuchoma moto kisichozidi TZS 2,000 kama itakavyokubaliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi;<br>i) Kutimiza masharti mengineyo yaliyowekwa kwenye kibali kama inavyoonekana kwenye **Jedwali la Kwanza.** |
| Kibali cha matumizi ya Moto kwa ajili ya shughuli za kiuchumi Vijijini | 6 | | Kibali cha matumizi ya Moto kwa ajili ya shughuli za kiuchumi Vijijini kinahusu matumizi ya moto katika shughuli za uchomaji wa matofali, uchomaji wa mkaa, urinaji wa asali na udhibiti wa uchomaji wa taka zitokanazo na mashine zinazohamishika na zisizohamishika za uchanaji wa mbao.<br><br>Mwombaji atatakiwa kukidhi masharti ya msingi yafuatayo:<br>a) Mwombaji ni sharti awe amesajiliwa katika Ofisi ya Serikali ya Kijiji/Mtaa;<br>b) Waombaji wengineo mbali na wawindaji na wavunaji asali, wanapaswa kuweka barabara za kuzuia moto zenye urefu wa nusu kipenyo cha Mita 15 kuzunguka maeneo yao ya kazi/eneo linalowaka moto;<br>c) Uwepo wa vifaa na zana za kuzimia au kudhibiti moto;<br>d) Kubainisha vyanzo maalum na vya kutosha vya maji;<br>e) Mwenye kibali au Mwakilishi aliyetajwa kwenye Kibali anapaswa kuwepo katika eneo ya uchomaji wa mkaa au matofali muda wote wa mchakato wa uchomaji akiwa na Wasaidizi wanne (4); |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | f) Kuwa tayari kuzitaarifu Mamlaka za Kijiji (Serikali ya Kijiji, Kamati na Kikosi) endapo kutatokea dharura yoyote ya moto.<br>g) Warinaji wa asali wanapaswa kutumia bomba la moshi na siyo kutumia moto kuchoma nyuki;<br>h) Kutimiza mahitaji mengineyo yaliyoambatanishwa kwenye kibali cha moto kama kinavyoonekana kwenye **Jedwali la Nne**. |
| Majukumu ya Mamlaka ya Serikali ya Mkoa | 7 | | Yafuatayo yatakuwa majukumu ya Mamlaka ya Serikali ya Mkoa katika kuzuia, kuratibu na kusimamia masuala ya moto wa msituni:<br>a) Kutoa sera, maelekezo ya kimkakati na sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto wa msituni;<br>b) Kuwezesha utekelezwaji wa sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto wa msituni katika Mamlaka za Halmashauri za Wilaya/Mji/Manispaa;<br>c) Kujenga uwezo wa kutosha kwa taasisi za kuzuia, kuratibu na kusimamia mot wa msituni;<br>d) Kuratibu na kusimamia utekelezwaji wa mikakati ya kuzuia na kusimamia moto wa msituni;<br>e) Kuwa kiunganishi chenye ufanisi wa mawasiliano kati ya Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa na Wakuu wa Wilaya husika katika masuala yote yanayohusu kuzuia na kusimamia moto wa msituni katika maeneo yao ya kiutawala;<br>f) Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuzuia na kusimamizi wa moto wa msituni;<br>g) Kufuatilia kwa karibu masuala yote ya moto wa msituni na kuwa kitovu cha kutunza takwimu zote za moto katika ngazi ya Mkoa;<br>h) Kuteua Afisa Mwandamizi atakayesimamia masuala yote yahusuyo moto wa msituni katika ngazi ya Mkoa na kutoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa. |
| Majukumu ya Halmashauri za Wilaya/ Miji/Manispaa | 8 | (1)<br><br>(2) | Kutakuwa na Kamati za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa za kuzuia, kuratibu na kusimamia moto wa msituni.<br><br>Kamati za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa za kuzuia na kusimamia moto wa msituni zitakuwa na jumla ya wajumbe kumi na nne (14) hadi kumi na tano (15) kulingana na idadi ya Tarafa zilizopo katika Halmashauri husika. Idadi hii ni nzuri |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ili kuweza kupata uwakilishi mpana kutoka kwa Wataalam wa Halmashauri/Miji/Manispaa na watoa maamuzi kwa upande mwingine. **Jedwali la Tano** linaonyesha vigezo vya kuzingatia wakati wa kuchagua wajumbe wa Kamati. |
| | | (3) | Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa kwa kushirikiana na Wakuu wa Idara ya Maliasili, Utalii na Mazingira watawajibika kuchagua Wajumbe wa Kamati ya kuzuia na kusimamia moto wa msituni katika maeneo yao ya kiutawala. |
| | | (4) | Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa kwa kushirikiana na Wakuu wa Idara ya Maliasili, Utalii na Mazingira watawajibika kuchagua Mjumbe mmoja ambaye ndiye atakuwa Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa. |
| | | (5) | Mkuu wa Wilaya atakuwa Mwenyekiti wa Kamati na Katibu wa Kamati atakuwa Mkuu wa Idara ya Maliasili, Utalii na Mazingira au Afisa Mwandamizi yeyote atakayeteuliwa na Mamlaka husika. |
| | | (6) | Majukumu ya kila siku ya Kamati ya Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa ya kuzuia, kudhibiti na kusimamia matumizi bora ya moto wa misituni yatafanywa na Waratibu wa Moto wa Misituni wa Halmashauri za Wilaya/Mji/Manispaa. |
| | | (7) | Kamati za kuzuia, kuratibu na kusimamia moto wa msituni katika Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa zitakuwa na majukumu yafuatayo:<br><br>a) Kuwa kiunganishi chenye ufanisi wa mawasiliano kati ya Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa na Wakuu wa Wilaya husika katika masuala yote yanayohusu kuzuia na kusimamia moto wa msituni katika maeneo yao ya utawala;<br>b) Kuunganisha Mamlaka za Kiutawala za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa na wadau wa kilimo cha miti; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | c) Kusaidia Serikali za Vijiji/Mitaa katika kutambua, kuwasiliana na kuwashirikisha Wawekezaji wa nje katika mipango ya Vijiji/Mitaa ya kuzuia kusimamia moto wa msituni;<br>d) Kusaidia Serikali za Vijiji/Mitaa kufungua Akaunti za Benki zinazojitegemea ili kuwezesha Mifuko ya Vijiji/Mitaa ya kuzuia na kusimamia moto wa msituni;<br>e) Kusaidia Serikali za Vijiji/Mitaa kuunda Kamati za Usimamizi wa Moto na Vikosi vya Kuzima Moto wa msituni;<br>f) Kufuatilia utendaji wa Kamati za Kusimamia Moto wa msituni katika Vijiji na Mitaa;<br>g) Kuhakikisha kwamba Maafisa Mtendaji wa Vijiji/Mitaa wanatoa vibali vya matumizi bora ya moto baada ya waomba Vibali kukaguliwa na Wajumbe wa Kamati kulingana na masharti yaliyoainishwa katika sheria Ndogo hizi;<br>h) Kufanya uchunguzi wa matukio ya moto na kuhakikisha kwamba sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto wa msituni zinatekelezwa ipasavyo;<br>i) Kuhakikisha kwamba Vijiji/Mitaa ina mipangokazi ya kuhamasisha wananchi juu ya utii wa sheria Ndogo za moto bila shuruti;<br>j) Kuandaa taarifa za matukio ya moto ya kila mwezi na kuziwasilisha katika Mamlaka za Mikoa;<br>k) Kuratibu shughuli zote za mafunzo yenye lengo la kuwajengea uwezo wananchi katika kuzuia na kusimamia moto wa msituni katika ngazi za Wilaya/Miji/Manispaa;<br>l) Kuratibu matukio ya uchangishaji fedha ili kuimarisha Mifuko ya Moto ya Vijiji/Mitaa.<br>m) Kufuatilia uendeshaji wa vituo vya hali ya hewa, ambavyo vinapaswa kuwekwa katika maeneo maalum kwa ajili ya kukokotoa Viashiria vya Hatari ya Moto (FDI);<br>n) Kuwasilisha Viashiria vya Hatari ya Moto (FDI) kila siku kwa Wananchi kupitia Mamlaka zao (Kamati, Kikosi na Serikali ya Kjijiji);<br>o) Kuwezesha programu za uhamasishaji juu ya majanga ya moto; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | p) Mratibu wa Moto wa Msituni Wilaya/Mji/Manispaa aliyeteuliwa atawajibika kufanya ukaguzi wa shughuli za kuzuiai na kusimamia moto wa msituni kwa kila Kijiji/Mtaa kila ifikapo tarehe 30 Juni ya kila mwaka ili kufahamu iwapo Vijiji/Mitaa inazingatia Mpangokazi wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji/Mtaa;<br>q) Kuwezesha ukaguzi wa mahesabu ya mwaka ya mfuko wa moto wa Kijiji/Mtaa.<br>r) Kusaidia mamlaka za Vijiji/Mitaa kushirikisha taasisi za elimu (Vyuo na mashule) katika kuhamasisha Wananchi juu ya kuzuia na kusimamia moto wa misituni kupitia michezo na burudani;<br>s) Kufanya kazi zote za kuzuiai na kusimamia moto wa msituni zitakazopangwa na Mamlaka za Mkoa. |
| Majukumu ya Kamati za Maendeleo ya Kata | 9. | | Majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) katika kudhibiti na kusimamia moto wa msituni yatakuwa kama kama yafuatavyo:<br>a) Kutatua migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi kati ya wawekezaji wa nje na wakazi;<br>b) Kuhakikisha kwamba Sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto wa misituni katika Vijiji/Mitaa zinatekelezwa ipasavyo;<br>c) Kupokea taarifa za kila mwezi za kuzuia na kusimamia moto wa msituni kutoka kwa Maafisa Mtendaji wa Vijiji/Mitaa au Mtu aliyeidhinishwa;<br>d) Kufuatilia utekelezaji wa mipangokazi ya usimamizi wa moto wa misituni katika Vijiji/Mitaa<br>e) Kuwasilisha taarifa za kila mwezi za kuzuia na kusimamia moto wa msituni kwa Mratibu wa Moto wa Msituni wa Wilaya/Mji/Manispaa. |
| Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Vijiji/Mitaa | 10. | (1) | Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Vijiji/ Mitaa katika kuzuia na kusimamia moto wa Msituni yatakuwa kama yafuatavyo:<br>a) Kuhakikisha kwamba Sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto wa msituni zinatekelezwa ipasavyo;<br>b) Kufanya mikutano ya uhamasishaji juu ya utii wa sharia za kuzuia na kusimamia moto wa msituni bila shuruti; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | c) Kuhamasisha Wananchi kushiriki katika masula ya kuzuia na kusimamia moto wa msituni kwa kushirikiana na Kamati na Kikosi;<br>d) Kushirikiana na Kamati ya kuzuia na kusimamia moto ili kuanzisha Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa;<br>e) Kufuatilia utekelezwaji wa Mpangokazi wa Kijiji/Mtaa wa kuzuia na kusimamia moto wa msituni;<br>f) Kuratibu shughuli za mafunzo kwa Kamati ya Usimamizi wa moto na Kikosi cha kuzima moto wa msituni;<br>g) Kushirikiana na Kamati ya Usimamizi wa moto ili kufungua Akaunti ya Benki inayojitegemea kwa ajili ya Mfuko wa moto wa Kijiji/Mtaa;<br>h) Kutatua au kutoa taarifa kwa Mamlaka za juu kuhusu uwepo wa migogoro itokanayo na matumizi ya misitu au matukio ya moto kati ya Wawekezaji wa misitu na Wananchi;<br>i) Kuhakikisha kwamba wakulima wote wa miti kijijini/Mtaa wamesajiliwa na kwamba wanazingatia matakwa ya sheria Ndogo hizi;<br>j) Kudumisha mawasiliano na Mamlaka za Vijiji/Mitaa jirani katika kubadilishana taarifa zinazohusu matukio ya moto;<br>k) Kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazotolewa na watoa taarifa kuhusu matukio ya uchomaji moto zinawekwa kuwa siri kuu;<br>l) Kuweka orodha ya zana na vifaa vya kuzimia moto na kuwa na mamlaka ya kuhakikisha kuwa vinatunzwa ipasavyo kwa matumizi ya dharura;<br>m) Kutoa ushauri kwa Kamati na Kikosi juu ya wajibu na majukumu yao.<br>n) Kuanzia mwezi wa NANE hadi mvua ya kwanza inapoanza kunyesha, Kamati ya kusimamia moto kwa kushirikiana na serikali ya Kijiji/Mtaa itahakikisha kwamba mikutano ya uhamasishaji inafanyika mara mbili kwa mwezi ili kutoa hamasa kwa wanajamii juu ya umuhimu wa kutii sheria Ndogo za kuzuia na kusimamia moto bila shuruti;<br>o) Kutoa Vibali vya moto na kuhakikisha kwamba masharti yote ya kibali yanazingatiwa; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | p) Kuandaa na kuweka mpakani mwa Kijiji/Mtaa mabango yanayokataza kuanzisha moto bila kibali;<br>q) Kuandaa na kuweka katikati ya Kijiji/Mtaa bango linaloonyesha rangi ya moto ya kila siku;<br>r) Kushirikisha taasisi za elimu (vyuo na mashule) katika kuhamasisha wananchi juu ya matumizi bora ya moto wakati wa majira ya moto;<br>s) Kutimiza majukumu yote ambayo yatatolewa na Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa. |
| | | (2) | Halmashauri ya Kijiji/Mtaa itatayarisha na kuweka alama za tahadhari ya moto kwenye mipaka ya Kijiji/Mtaa |
| | | (3) | Alama zitakazowekwa ni kwa mujibu wa Kifungu cha 2 cha Ibara hii na zitaundwa kama ifuatavyo:- **TAHADHARI!TAHADHARI!**<br><br>**SASA UNAINGIA KATIKA KIJIJI/MTAA CHA/WA…………………………………………………… NI MARUFUKU KUWASHA MOTO BILA KIBALI. PIA UNA WAJIBU WA KUTOA TAARIFA KUHUSU TUKIO/MATUKIO YOYOTE YA UWEPO WA MOTO NA KUSHIRIKI KATIKA KUZUIA NA KUUDHIBITI MOTO WA MSITUNI.** |
| Majukumu ya Kitongoji | 11 | | Yafuatayo yatakuwa majukumu ya Kitongoji katika kuzuia na kusimamia moto wa msituni:<br>a) Kutambua wawekezaji wote wa nje kwenye sekta ya misitu ndani ya Kitongoji;<br>b) Kutambua Makundi Maalumu ya watu wanaojihusisha na matumizi ya moto kwenye shughuli zao za kibiashara (Uchomaji mkaa, Upasuaji wa mbao, Uchomaji wa matofali, Urinaji wa asali na Uwindaji wa wanyama);<br>c) Kusimamia utekelezwaji wa mpangokazi wa Usimamizi wa moto wa Kijiji/Mtaa;<br>d) Kuhakikisha kwamba wenye vibali vya kutumia moto wanazingatia masharti yote yaliyoainishwa kwenye vibali vyao;<br>e) Kusaidia uchunguzi juu ya matukio ya moto Kijijini/ kwenye Mtaa; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | f) Kuhimiza wakazi wa Kitongoji kutoa taarifa za uwepo wa matukio ya moto;<br>g) Kuhakikisha kwamba Kitongoji kinafanya mikutano juu ya masuala ya moto wa msituni mara mbili kila mwezi wakati wa kipindi cha majira ya moto kuanzia mezi wa Nane hadi mvua ya kwanza inapoanza kunyesha. |
| Kamati ya Kijiji/Mtaa ya Kusimamia Moto wa Msituni | 12 | | Kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi, Halmashauri za Kijiji/Mtaa zitachagua wajumbe wa Kamati za Kusimamia Moto wa Msituni. Wajumbe hao ni sharti wapitishwe na Mkutano Mkuu wa Kijiji/Mtaa. |
| Muundo wa Kamati | 13<br>. | | Kamati itakuwa na wajumbe wafuatao; -<br>a) Mwenyekiti wa Kamati atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Kamati;<br>b) Katibu wa Kamati pia atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Kamati<br>c) Majukumu ya kila siku ya Kamati yatatekelezwa na Wajumbe wa Kamati;<br>d) Wenyeviti wote wa Vitongoji watakuwa Wajumbe wa Kamati;<br>e) Wajumbe watano (5) wa nyongeza ambao watachaguliwa ili kuwakilisha makundi mbalimbali Kijijini/Mtaa kwa kuzingatia masula ya jinsia, umri, kazi na kabila;<br>f) Uwakilishi wa kamati kuu ya TGA;<br>g) Kamati itakuwa na jumla ya Wajumbe 25. Idadi hii inachukuliwa kuwa ya kutosha ili kupunguza mzigo kwa kamati hasa wakati wa ukaguzi wa mashamba kwa waombaji wa vibali.<br>h) Kiutawala, Kamati ya kusimamia Moto wa msituni itawajibika kwa Serikali ya Kijiji/Mtaa. |
| Majukumu ya Kamati ya Kijiji/Mtaa ya Kusimamia | 14 | (1) | Kutakuwa na Kamati ya Kijiji/Mtaa ya kusimamia moto wa msituni. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Moto wa Msituni | | (2) | Kamati ya Kijiji/Mtaa ya kusimamia moto wa msituni itafanya majukumu yafuatayo:-<br>a) Kuandaa Mpangokazi wa kusimamia moto wa msituni kwa kushirikiana na Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri/Mji/Manispaa;<br>b) Kusimamia utekelezwaji wa mpangokazi wa kusimamia wa moto wa msituni;<br>c) Kusimamia Kikosi cha Kuzima Moto cha KijijiMtaa;<br>d) Kusimamia Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa;<br>e) Kuhamasisha jamii kuhusu fahirisi ya Hatari ya Moto (FDI) na maana yake juu ya matumizi ya moto;<br>f) Kudumisha mawasiliano na Vijiji/Mitaa jirani kuhusu masuala ya moto;<br>g) Kudhibiti matumizi ya vifaa vya kuzimia moto na kuhakikisha kwamba vifaa vilivyopo vinapata matengenezo ya kila mara;<br>h) Kuchukua sense ya kila mwaka ya vifaa vilivyopo ili kubaini mapungufu ya vifaa vinavyohitajika ili kufanya zoezi la kuzima moto liwe la ufanisi;<br>i) Kuhamasisha Wananchi juu ya ushiriki wao katika kuzuia na kusimamia moto wa msituni;<br>j) Kutoa mapendekezo kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa au Mamlaka ya uwakilishi wakati wa kutoa vibali vya kutumia moto baada ya kujiridhisha kuwa maombi ya vibali hivyo yamekidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;<br>k) Kusaidia uchunguzi juu ya matukio ya moto Kijijini/Mtaa;<br>l) Kutunza kumbukumbu za matukio yote ya moto na kutoa taarifa za kila mwezi kwa Mamlaka za Serikali ya Kijiji/Mtaa husika; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | m) Kutunza kumbukumbu zote ikiwa ni pamoja na rejisita ya kila siku ya FDI, hali ya hewa, vifaa vya kuzimia moto, vibali vya moto na matukio ya moto Kijijini/Mtaa;<br>n) Kuhakikisha kwamba ubao unaoonyesha rangi za moto Kijijini/Mtaa unabadilishwa kila siku kama ilivyopangwa;<br>o) Kufanya kazi nyinginezo zinazohusiana na usimamizi wa moto wa msituni kama zinavyoonyeshwa kwenye Mpangokazi wa Kijiji/Mtaa wa kusimamia moto wa msituni au kama zitakavyotolewa na Serikali ya Kijiji/Mtaa au kama zitakavyotolewa na Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa. |
| | | (2) | Katika kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi, wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Moto katika Kijiji/Mtaa hawatawajibika binafsi kwa hatua/shughuli/maamuzi yoyote yatakayofanyika wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. |
| | | (3) | Hata hivyo, itakuwa ni kosa kwa mjumbe wa Kamati kutekeleza majukumu yake kwa uzembe. |
| | | (4) | Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote kumshinikiza shahidi asitoe ushahidi mahakamani au kutoa taarifa katika kituo cha polisi au ofisi nyingine anapotakiwa kufanya hivyo; |
| | | (5) | Kwa mujibu wa sheria ndogo hizi, hautokuwepo utetezi kwamba shahidi hakufika mahakamani au kituo cha polisi au ofisi nyingine kwa sababu ya kukosa usafiri. |
| | | (6) | Kamati itafanya vikao vyake kila mwezi hata wakati wa kipindi cha masika. |
| | | (7) | Taarifa kutoka kwa Kamati itatumwa kwa Mratibu wa Moto wa Msituni wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa kwa kufuata |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | mfumo wa Kiserikali wa mawasiliano yaani kupitia kwa Mtendaji wa Kata ambaye hufanya shughuli za kila siku za Kamati za Maendeleo ya Kata |
| | | (8) | Posho za vikao vya Kamati zitapangwa na Halmashauri ya Kijiji/Mtaa na zitatoka kwenye Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa ambao utaanzishwa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi. |
| | | (9) | Bila kuathiri kifungu chochote cha sheria Ndogo hizi au sheria nyingine yoyote inayotumika nchini Tanzania, Wajumbe wa Kamati watahudumu kwa muda wa miaka mitatu (3) kuanzia tarehe ya uteuzi na wanaweza kuteuliwa tena. |
| Kikosi cha Kuzima Moto cha Kijiji/Mtaa | 15 | (1)<br>(2) | Kutakuwa na Kikosi cha Kuzima Moto cha Kijiji/Mtaa.<br>Yafuatayo yatakuwa ni majukumu ya Kikosi:<br>a) Kuandaa barabara kuu za kuzuia moto holela kuzunguka mipaka ya Kijiji/Mtaa na kugawa mashamba makubwa ya miti kulingana na Mpango kazi wa Usimamizi wa Moto wa Kijiji/Mtaa<br>b) Kufanya doria ya kuangalia moto kwa mbali, kufuatilia maeneo yaliyochomwa moto hivi karibuni na kuwa tayari wakati wowote kwenda kuzima moto pindi utokeapo.<br>c) Kushauri watu wenye mashamba juu ya matumizi bora ya moto wakati wa kuandaa mashamba yao.<br>d) Kuwa Watu wa kwanza kufika kwenye tukio pindi moto utokeapo Kijijini/Mtaa.<br>e) Pindi moto utokeapo, Kikosi kitahakikisha kwamba moto wote umezimwa kabisa na baada ya hapo, Kikosi kitaendelea kufuatilia moto huo kwa muda wa siku saba (7) iwapo taka zilizochomwa moto ni matawi na masalia ya shughuli za viwanda vya kupasua mbao. Lakini kama taka zilizochomwa moto ni nyasi au masalia ya taka za shambani, Kikosi kitafuatilia |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | mwenendo wa moto huo kwa muda wa siku mbili (2) kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.<br>f) Kudumisha mawasiliano na Kamati ya Kusimamia Matumizi Bora ya Moto ya Kijiji/Mtaa.<br>g) Kuhakikisha kwamba vifaa na zana za kuzimia moto zinafanyiwa matengenezo na kutunzwa katika mazingira salama kama itakavyoshauriwa na Kamati ya Kusimamia Matumizi Bora ya Moto ya Kijiji/Mtaa;<br>h) Kutekeleza majukumu ya kuzuia na kudhibiti moto kama itakavyoelekezwa na Kamati ya Usimamizi wa Matumizi Bora ya Moto ya Kijiji/Mtaa. |
| Muundo wa Kikosi cha kuzima moto cha Kijiji/Mtaa | 16 | | Kila Kikosi cha kuzima moto cha Kijiji/Mtaa kitakuwa na wajumbe angalau 15. Kijiji/Mtaa kinaweza kuwa na Kikosi zaidi ya kimoja kutokana na ukubwa wake au jiografia yake. |
| | | | Kikosi kitaongozwa na Kamanda ambaye atakuwa na sifa na uwezo wa kiuongozi na ambaye amefunzwa kikamilifu jinsi ya kupambana na majanga ya moto wa msituni |
| Vigezo vya kuchagua Wajumbe wa Kikosi cha kuzima moto cha Kijiji/ Mtaa | 17 | | Vigezo vya kuchagua wajumbe wa Kikosi ni kama vifuatavyo;<br>a) Awe mtu mwenye afya njema na ustahimilivu wa mwili;<br>b) Utayari wa kufanya kazi za kujitolea kwa muda mrefu na kuwa katika hali ya kupambana na moto pindi utokeapo;<br>c) Uwakilishi wa kila Kitongoji;<br>d) Kuwa katika mazingira ya utayari wa kupambana na moto muda wowote wakati wa msimu hatari wa moto;<br>e) Kipaumbele kitatolewa kwa wale ambao wamepitia mafunzo ya kuzima moto;<br>f) Nidhamu nzuri na utayari wa kupokea maagizo mara moja. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa | 18 | (1)<br>(2) | Kutakuwa na Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa<br>Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa utaanzishwa na Serikali ya Kijiji/Mtaa kwa ajili ya kutekeleza mpangokazi wa kuzuia na kusimamia moto wa msituni Kijijini/Mtaa. |
| | | (3) | Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa utafanya kazi kulingana na andiko la Mpango kazi wa Usimamizi wa Moto. Vyanzo vya mapato ya Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa vitaanishwa katika andiko la Mpango kazi wa Usimamizi wa Moto na kupitiwa kila mwaka. Kwa uchache, miongoni mwa vyanzo vinavyopendekezwa ni pamoja na:<br>a) Faini zinazolipwa nawahalifu kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi;<br>b) Michango itakayokusanywa na kamatiya usimamizi wa matumizi bora ya moto kutoka kwa wafanya biashara wa mazao ya misitu ambao kwa namna moja au nyingine hawahusiki na shughuli za kuzuia na kudhibiti moto moja kwa moja katika Kijiji/Mtaa;<br>c) Michango itakayokusanywa kutoka kwa wawekezaji wa nje kama ilivyoainishwa chini ya Jedwali la Pili la sheria Ndogo hizi;<br>d) Ruzuku kutoka Serikali ya Kijiji/Mtaa au Halmashauri;<br>e) Ufadhili kutoka kwa wadau mbalimbali.<br>f) Misaada kwa Kamati kutoka kwa watu na taasisi mbalimbali, |
| | | (3) | Pesa kwa ajili ya mfuko moto wa Kijiji /Mtaa zitakusanywa na Mamlaka ya Serikali ya Kijiji/Mtaa na kuwekwa kwenye mfuko wa moto wa Kijiji/Mtaa mara moja. |
| | | (4) | Mfuko wa moto wa Kijiji/Mtaa utakuwa na watia saini walioteuliwa na Halmashauri ya Kijiji/Mtaa. Angalau mtia saini mmoja atakuwa mjumbe wa Kamati yaUsimamizi wa Matumizi Bora ya Moto ya Kijiji/Mtaa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (5) | Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa utatumika kwa ajili ya kutekeleza mpangokazi wa usimamizi wa matumizi bora ya moto wa msituni. |
| | | (6) | Mkaguzi wa ndani wa Wilaya/Mji/Manispaa atafanya ukaguzi wa mahesabu ya Mfuko wa moto kila mwaka. |
| Wajibu wa jamii katika kuzuia i na kusimamia moto wa msituni | 19 | (1) | Litakuwa ni jukumu la kila mwanajamii kuzuia moto na kushiriki katika kuzima moto. |
| | | (2) | Katika kuzuia na kudhibiti vitisho vya moto, kila mwanajamii anapaswa kuzingatia yafuatayo:<br>a) Kuhudhuria mikutano ya uhamasishaji wa kuzuia na kusimamia moto;<br>b) Kutumia njia mbadala mbali na matumizi ya moto wakati wa maandalizi ya mashamba, kurina asali na kuwinda wanyama;<br>c) Kuzingatia sheria Ndogo hizi, pamoja na kufuata taratibu za kitalaamu katika shughuli zao za kila siku.<br>d) Kuzingatia mpangokazi wa Kijiji/Mtaa wa usimamizi wa moto wa msituni. |
| Makosa | 20 | (1) | Mtu yeyote atakayekiuka sheria Ndogo hizi atakuwa anatenda kosa na akipatikana na hatia ataadhibiwa kwa yafuatayo:-<br>a) Kuwasha moto bila kibali cha kutumia moto kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi;<br>b) Kuwasha moto ambao utakuwa hatari na kusababisha hasara ya mali au majeraha au kupoteza maisha;<br>c) kutofuata masharti katika kibali cha kutumia moto;<br>d) Kukosa kuripoti moto au moshi kwa Mamlaka husika;<br>e) Kukataa au kupuuza kushiriki katika shughuli za kuzima moto;<br>f) Kumshawishi mtu mwingine asishiriki katika kuzima moto; |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | g) Kushindwa kuweka barabara za kuzuia moto kuzunguka eneo la ardhi/shamba kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi;<br>h) Mjumbe wa Kamati au Kikosi kushindwa kuwajibika ipasavyo bila sababu yoyote ya msingi;<br>i) Kufanya kitendo chochote kinachokinzana na sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Katika hatua za awali, Mtuhumiwa atafikishwa katika ofisi ya serikali ya Kijiji/Mtaa na kuelezwa anachotakiwa kushtakiwa nacho. Iwapo atakiri kosa na kukiri kwa kujaza fomu kama ilivyoainishwa chini ya **Jedwali la Sita** la sheria Ndogo hizi, atatakiwa kulipa faini kwa kiwango kilichopangwa chini ya sheria Ndogo hizi.<br>Katika kesi ambayo mshitakiwa hatakiri mashitaka yake atapelekwa kwenye Baraza la Usuluhishi wa Migogoro ambapo akipatikana na hatia atalipa faini na fidia kwa usumbufu utakaojitokeza. |
| Adhabu | 21 | | Mtu yeyote atakayekiuka sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia adhabu yake itakuwa kwa mujibu wa **Jedwali** la **Tatu** la sheria Ndogo hizi. |
| Kufifia kosa | 22 | | Afisa Mtendaji au Afisa Mfawidhi atakuwa na uwezo wa kumtoza mhalifu kiasi kisichozidi Shilingi milioni moja za Kitanzania (1,000,000) pale mkosaji anapokiri kosa lake kwa kujaza hati iliyoainishwa chini ya **Jedwali la Sita** la sheria Ndogo hizi . |

Muhuri wa Halmashauri ya Kijiji/Mtaa cha ……………………… uligongwa kwenye hati ya Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la Mkutano Mkuu wa Serikali ya Kijiji/Mtaa uliofanyika tarehe…………. Mwezi……. mwaka ……… na uligongwa kwa kushuhudiwa na:

**........................................** **........................................**

Saini na Muhuri wa

**MWENYEKITI WA KIJIJI/MTAA**

Saini na Muhuri wa

**AFISA MTENDAJI**

**IMEIDHINISHWA NA:**

**..........................................................**
**MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA**

**..................................……**
**MKURUGENZI MTENDAJI (H) WILAYA**

## JEDWALI LA KWANZA

(Imeundwa chini ya kifungu cha 4(3)

**SHERIA NDOGO ZA KUZUIA NA KUSIMAMIA MOTO WA MSITUNI ZA HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA /WA................................................ YA 2022**

**HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA/WA --------- ----------------------KATA--------------**

## KIBALI CHA KUTUMIA MOTO

**A: UTANGULIZI NA MAWASILIANO**

1. Namba ya simu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa -----------------------------------------
2. Namba ya simu ya Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa ------------------------------------------- ---
3. Namba ya simu ya Mwenyekiti wa Kamati ------------------------------------------- --
4. Namba ya simu ya Kamanda wa Kikosi------------------------------------------ -----------
5. Namba ya simu ya Mwenyekiti wa Kitongoji ----------------------------------------------
6. Namba ya simu ya Mwombaji wa Kibali --------------------------------------------------
7. Tarehe ya Kibali ---------------------------------------------------------------------------------
8. Nambari ya Kibali --------------------------------------------- -----------------------------------
9. Shamba liko Kitongoji gani? ------------------------------------------------------------------
10. Kibali kimetolewa kwa: ------------------------------------------ --------------------------------

**B: KUSUDI LA KUTUMIA MOTO**: ---------------------------------------- --------------------------

**C: UKAGUZI WA ENEO**

1. Je, FDI itakuwa chini ya 55 kwa siku 3 mfululizo? **NDIYO/HAPANA**
2. Je, kuna barabara za kuzuia moto kuzunguka shamba lake? **NDIYO/HAPANA**
3.Je, Majirani na shamba lengwa wamejulishwa angalau siku tatu kabla?**NDIYO/HAPANA**
4. Je, taka hizo zina sifa ya kuchomwa moto? **NDIYO/HAPANA**
5. Je, shamba hilo liko kwenye mwinuko? **NDIYO/HAPANA**

**D. ORODHESHA VIFAA VYA KUZIMIA MOTO VILIVYOPO:**

I. ------------------------------------- II. ------------------------------ . III. ------------------------------
IV. -------------------------------------. V. ------------------------------. VI. ---------------------------

**E: MAJINA YA WASAIDIZI NA NAMBA ZAO ZA SIMU**

1. ------------------------------------------- -------- 2. ------------------------------------- --------------
3. -------------------------------------------- -------- 4. ------------------------------------- -------------
5. ------------------------------------------- ----------6. ----------------------------------------------- ---

**F: MASHARTI YAFUATAYO YANAPASWA KUZINGATIWA**

i. Wakati unaoruhusiwa kuchoma moto ni baada ya saa 12 jioni.
ii. . Eneo lazima lilindwe na kuangaliwa kwa siku 7 mfululizo ikiwa ni shamba la miti na siku 2 kwa eneo lenye taka za kawaida za shambani.
iii. Kama itatokea hali ya hewa isiyotarajiwa, ulinzi na doria ni lazima ufanyike katika eneo hilo. Pia ni vyema walinzi wawe na simu kwa ajili ya mawasiliano.
iv. Iwapo moto utatoroka, viongozi waliotajwa hapo juu ni lazima wafahamishwe.
v. Kutofuata masharti yaliyowekwa kwenye Kibali hiki kunaweza kupelekea hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yako.

**G: UKAGUZI WA SHAMBA NA MAMLAKA YA IDHINI YA VIBALI**

Shamba lilikaguliwa na: ---------------------------------------- Tarehe: ------------------

**MJUMBE WA KAMATI**

Kibali kilitolewa na: ------------------------------------------ -- Tarehe na Kisiki --------------------

**AFISA MTENDAJI WA KIJIJI/ MTAA**

## JEDWALI LA PILI

(Imeundwa chini ya kifungu cha 18 (c)

**SHERIA NDOGO ZA KUZUIA NA KUSIMAMIA MOTO WA MSITUNI ZA HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA /WA................................................. YA 2022**

**HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA/WA --------- -----------------------KATA----------------**

**MICHANGO YA KILA MWAKA KUTOKA KWA WAWEKEZAJI WA NJE**

| **Na.** | **Ukubwa wa Shamba (Ha)** | **Kiasi cha mchango/mwaka** |
|---|---|---|
| 1 | 1 - 30 | 25,000 |
| 2 | 31 - 50 | 50,000 |
| 3 | 51 - 100 | 150,000 |
| 4 | 101 - 200 | 200,000 |
| 5 | 201 - 500 | 250,000 |
| 6 | $501^{+}$ | 1,000,000 |

## JEDWALI LA TATU

(Imeundwa chini ya kifungu cha 21(1)

**SHERIA NDOGO ZA KUZUIA NA KUSIMAMIA MOTO WA MSITUNI ZA HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA /WA................................................ YA 2022**

**HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA/WA --------- ----------------------KATA----------------**

### MAKOSA NA ADHABU

| Kosa | Adhabu |
|---|---|
| a) Kuwasha moto bila kibali cha kutumia moto kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. | TZS 50,000 hadi 1,000,000, kifungo au Vyote viwili. |
| b) Kuwasha moto ambao utakuwa hatari na kusababisha hasara ya mali au majeraha au kupoteza maisha. | Mmiliki/mmiliki wa kukodisha atafidiwa hasara ya mali aliyopata kulingana na ripoti rasmi za uthaminishaji.<br>Sheria za nchi zitatumika kuangalia fidia itakayolipwa mtu endapo atapoteza maisha au kupata majeraha. |
| c) Kushindwa kufuata masharti yaliyowekwa kwenye Kibali cha kuchoma moto. | TZS 50,000 hadi 1,000,000, kifungo au Vyote viwili. |
| d) Kushindwa kutoa taarifa juu ya uwepo wa moshi au moto kwa Mamlaka ya Kijiji/Mtaa. | TZS 5000 hadi 50,000 |
| e) Kukataa au kupuuza kushiriki katika shughuli za kuzima moto. | TZS 50,000, kifungo au Vyote viwili |
| f) Kumshawishi mtu mwingine asishiriki katika kuzima moto. | TZS 50,000, kifungo au Vyote viwili |

| | |
|---|---|
| g) Kushindwa kuweka barabara za kuzuia moto kuzunguka eneo /shamba kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. | TZS 50,000 hadi 1,000,000, kifungo au Vyote viwili. |
| h) Mjumbe wa Kamati au Kikosi kushindwa kutenda kazi zake kwa uwajibikaji bila sababu yoyote ya msingi. | TZS 50, 000 |
| i) Kushindwa kusimamia vyema mashamba ya miti ya kupandwa. | TZS 50,000 hadi 1,000,000, kifungo au vyote kwa pamoja. |
| j) Kushindwa kuchangia Mfuko wa Moto wa Kijiji/Mtaa kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi | Atatakiwakutozwa faini ya malipo mara mbili ya kiwango kinachopendekezwa kwenye Jedwali la Pili kulingana na ukubwa wa uwekezaji wake |
| k) Kukosa kuhudhuria mikutano mitatu mfululizo ya usimamizi wa moto | TZS 1,000 hadi 5,000 |

**JEDWALI LA NNE**

(Imeundwa chini ya kifungu cha 6(h)

**SHERIA NDOGO ZA KUZUIA NA KUSIMAMIA MOTO WA MSITUNI ZA HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA /WA................................................ YA 2022**

**HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA/WA --------- ----------------------KATA----------------**

**KIBALI CHA KUCHOMA MKAA, MATOFALI NA KUTUMIA MOTO KWENYE MAKAMBI YA KUPASUA MBAO**

**A: MAWASILIANO**

1. Namba ya Simu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa------------------------------------------
2. Namba ya Simu ya Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa ---------------------------------------------
3. Namba ya Simu ya Mwenyekiti wa Kamati -----------------------------------------------
4. Namba ya Simu ya Kamanda wa Kikosi-----------------------------------------------------
5. Namba ya Simu ya Mwombaji wa Kibali -------------------------------------------------
6. Namba ya Simu ya Mwenyekiti wa Kitongoji ---------------------------------
7. Tarehe ya kuomba Kibali ------------------------------------------------------------------
8. Shughuli hii itafanyika katika Kitongoji gani? ----------------------------------------------
9. Karibu na kitu gani cha Kijiografia au Mtu Maarufu-----------------------------------------
10. Nambari ya Kibali ----------------------------------------------------------------------------
11. Kibali kimetolewa kwa: --------------------------------------------------------------------

**B: MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA KIBALI**

1. Wachoma Mkaa, Matofali au watumia moto kwenye makamabi ya kupasualia mbao ni sharti kwanza wajiandikishe katika Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa kabla ya kuanza kazi zao za uzalishaji. Lengo la kujiandikisha ni kufahamu idadi yao na kutambua maeneo yao ya kazi ili iwe rahisi kwa Kamati kuwatembelea na kuwakagua.
2. Wachoma Mkaa, Matofali au watumia moto kwenye makamabi ya kupasualia mbao ni sharti waweke barabara za kuzuia moto zenye urefu wa nusu Kipenyo cha Mita 15 kuzunguka matanuri yao au maeneo ya kupikia wapasua mbao.
3. Watajwa hapo juu, ni sharti wawe na vifaa na zana za kuwasaidia kuzima moto endapo utaonyesha dalili za kutoroka.

4. Wachoma Mkaa, Matofali au watumia moto kwenye makambi ya kupasua mbao wanatakiwa kuhakikisha kuwa wamefukia kuni za mkaa au matofali kwa udongo wa kutosha ili kuzuia uwezekano wa matanuri yao kulipuka.
5. Wachomaji wa Mkaa na Matofali wenye vibali watalazimika muda wote kuwa karibu na matanuri yao ili kufuatilia mwenendo wa uunguaji wa tanuri zao.
6. Litakuwa ni kosa kwa mwenye kibali cha kuchoma Mkaa au Matofali kutokuwepo jirani na tanuru lake hata kama moto hauonyeshi dalili zozote za kutoroka.
7. Wachoma Mkaa, Matofali au watumia moto kwenye makambi ya kupasua mbao siku ya kumaliza shughuli zao katika maeneo yaliyoombewa kibali ni lazima wahakikishe kwamba hakuna dalili zozote za uwepo wa moto. Hata hivyo, kabla ya kuondoka katika eneo la kazi ni **LAZIMA** wakaguliwe na Kamati kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi.
8. Kupuuzia masharti yoyote yaliyoainishwa katika kibali hiki kunaweza kusababisha hatua za kisheria kuchukulia dhidi yako.

**C: UKAGUZI WA MWOMBAJI KIBALI NA ENEO LA KUFANYIA KAZI**

1. Je, mwombaji wa kibali amesajiliwa kwenye ofisi ya Kijiji? **NDIYO/HAPANA**
2. Je, mwombaji wa kibali ametengeneza barabara ya kuzuia moto yenye upana wa Mita 15 ya kipenyo kuzunguka eneo lake ya shughuli? **NDIYO/HAPANA**
3. Je, eneo hilo liko karibu na chanzo chochote cha maji? **NDIYO/HAPANA**
4. Je, mwombaji wa Kibali ni mzoefu katika shughuli anyoombea Kibali? **NDIYO/HAPANA**

D. **ORODHESHA VIFAA VYA KUZIMIA MOTO UTAKAVYOCHUKUWA**

I. -------------------------II. ----------------------------- III. ----------------------------------------

**E: ORODHESHA MAJINA YA WASAIDIZI NA NAMBA ZAO ZA SIMU**

1. -------------------------------------------------------------------------------------------------------------
2. -------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**F: UKAGUZI WA ENEO LA KAZI NA MAMLAKA YA KIBALI**

Eneo limekaguliwa na: **------------------------------ ----------------- ---------------------**

**MJUMBE WA KAMATI Sahihi Tarehe**

Kibali kimetolewa na: **--------------------------------------------- Tarehe na Mhuri ----------------**

**AFISA MTENDAJI WA KIJIJI**

**JEDWALI LA TANO**

(Imeundwa chini ya kifungu cha 8(2)

**SHERIA NDOGO ZA KUZUIA NA KUSIMAMIA MOTO WA MSITUNI ZA HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA /WA................................................ YA 2022**

**HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA/WA --------- -----------------------KATA----------------**

**VIGEZO VYA KUCHAGUA WAJUMBE WA KAMATI YA MOTO YA HALMASHAURI**

| Na. | Halmashauri/Wilaya | Wajumbe kutoka Wilayani | Idadi ya Maafisa Tarafa waliopo | Wenyeviti wa Halmashauri | Maafisa Watendaji Kata | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilolo DC | 8 | 3 | 1 | 3 | 14 |
| 2 | Mafinga TC | 8 | 2 | 1 | 4 | 14 |
| 3 | Mufindi DC | 8 | 5 | 1 | 1 | 14 |
| 4 | Makambako TC | 8 | 1 | 1 | 5 | 14 |
| 5 | Wanging'ombe DC | 8 | 3 | 1 | 3 | 14 |
| 6 | Makete DC | 8 | 6 | 1 | 0 | 15 |
| 7 | Njombe DC | 8 | 2 | 1 | 4 | 14 |
| 8 | Njombe TC | 8 | 2 | 1 | 4 | 14 |
| 9 | Madaba DC | 8 | 1 | 1 | 5 | 14 |
| 10 | Ludewa DC | 8 | 5 | 1 | 1 | 14 |

**Orodha ya Wajumbe wa Kamati ya moto kutoka Makao Makuu ya Wilaya/Halmashauri**

i. Mkuu wa Wilaya — **Mwenyekiti**
ii. Mhifadhi wa Misitu Wilaya (TFS) — Mjumbe
iii. Mkuu wa Jeshi la Zimamoto Wilaya — Mjumbe
iv. Mkuu wa Kitengo cha Moto Sao hill/TFS — Mjumbe
v. Afisa Mazingira wa Halmashauri — Mjumbe

| | | |
|---|---|---|
| vi. | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii | Mjumbe |
| vii. | Mkuu wa Idara ya Maliasili, Utalii na Mazingira | **Katibu** |
| **viii.** | Afisa Misitu | **Mratibu wa Moto wa Msituni wa (H)** |

## JEDWALI LA SITA

(Imeundwa chini ya kifungu cha 22)

**SHERIA NDOGO ZA KUZUIA NA KUSIMAMIA MOTO WA MSITUNI ZA HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA /WA.................................................. YA 2022**
**HALMASHAURI YA KIJIJI/MTAA CHA /WA......................... KATA ----------------------**

## HATI YA KUKIRI KOSA

Mimi …………………………………………. kwa hiari yangu mwenyewe ninakiri kosa mbele …………………………………………………………ambaye ni Afisa aliyeidhinishwa wa Kijiji/Mtaa kwamba tarehe ……… ya mwezi……………………. mwaka………. nilifanya kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu.…………………. cha sheria Ndogo za kuzuia na kudhibiti moto za Kijiji/Mtaa cha/wa............................... za mwaka 2022. Niko tayari kulipa faini ikiwa Afisa aliyeidhinishwa ataamua kutekeleza Mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo hizi. Ninathibitisha kwamba maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli, na kwamba nimeyatoa kwa hiari yangu mwenyewe kwa kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe ……………… mwezi …………………… mwaka.......................

Jina ……………………………………………………

Sahihi……………

Alikiri kosa mbele ya:

Jina ………………………………………………………

Cheo ………………………………………………….

Sahihi ……………………

Tarehe………………………………

Indufor ...forest intelligence

NIRAS